King County

# Vipaumbele vya mwaka 2024 vya Bunge la Jimbo kwa Watoto wenye Uchelewaji wa Makuzi na Watu wenye Ulemavu wa Akili na/au Makuzi.



www.kingcounty.gov/ddecsd

***Huduma kwa watu wenye uchelewaji wa makuzi na ulemavu wa akili na/au makuzi (I/DD) zinapaswa kuwa endelevu na kuzingatia usawa, ujumuishaji, na kukubalika. Vipaumbele vya mwaka 2024 vinalenga kufikia dira hii na kuakisi mawazo ya jumuiya iliyoathiriwa katika kanda yote, vikiweka mkazo kwa watu wenye uchelewaji na ulemavu, na Weusi, Wazawa, na Watu wenye Rangi (BIPOC).***

## VIPAUMBELE

### KIPAUMBELE CHA 1
Kusaidia kuhakikisha kwamba watu binafsi na familia zinapata huduma zinazotolewa na watu wanaozungumza lugha yao na wanaozingatia mahitaji ya tamaduni zao.

### KIPAUMBELE CHA 2
Kusaidia kuhakikisha mashirika ya Usaidizi wa Awali wa Watoto Wachanga na Watoto Wadogo (ESIT) yanapata ufadhili wa Elimu Maalum kwa mwezi wa kwanza wa huduma zinazotolewa kwa familia.

### KIPAUMBELE CHA 3
Kusaidia watu wenye I/DD kupata ajira na kudumu kazini, na kushirikishwa katika jumuiya zao, kwa kuongeza kiasi wanacholipwa watoa huduma za Ajira na Ujumuishaji katika Jumuiya.

### KIPAUMBELE CHA 4
Kusaidia kuhakikisha nyumba za gharama nafuu, na huduma ya usaidizi wa nyumba, zinapatikana kwa watu wenye I/DD.

### KIPAUMBELE CHA 5
Kuajiri watoa huduma zaidi wa afya ya tabia na kuwapa mafunzo ya utaalamu wa kuhudumia kwa ufanisi zaidi watu wenye I/DD.

2310_13388R_DevelopDisabLegisForum.ai

## KIPAUMBELE CHA 1 – Ufikio wa Lugha

Kusaidia kuhakikisha kwamba watu binafsi na familia zinapata huduma zinazotolewa na watu wanaozungumza lugha yao na wanaozingatia mahitaji ya tamaduni zao.

Ufikio wa lugha ni muhimu katika mifumo na programu zote ili kuhakikisha kwamba kila mtu anaweza kufikia huduma bila kujali anazungumza lugha gani. Ni muhimu pia kwamba huduma zizingatie utamaduni wa familia. Watu na familia hunufaika na huduma wanazopata kutoka kwa watoa huduma wenye tamaduni, historia, imani, na lugha zinazofanana na zao. Hii inamaanisha huduma wanazopata ni muhimu, zinaendana, saidizi na hazina upendeleo.




Kutafsiri nyaraka mbalimbali za huduma katika lugha pendwa ya kila mtu binafsi na kila familia ni muhimu sana, lakini pia ni aghali. Hii pia inahusika kwa wakalimani, ambao si wakati wote wanakingwa na bima. Bunge linaweza kuendeleza ubora wa huduma ambazo watu binafsi na familia wanazistahili kwa kufadhili ufikio wa lugha kwa mashirika ya jimbo, ikiwemo Shirika la Usimamizi wa Ulemavu wa Makuzi (DDA), Idara ya Watoto, Vijana na Familia (DCYF), Divisheni ya Urekebishaji kupitia Ufundi (DVR), na Mamlaka ya Huduma ya Afya (HCA).



**Wakazi wenye ulemavu ambao pia ni Weusi, Wazawa, na Watu wenye Rangi wameiambia King County kwamba wanapata shida kukidhiwa mahitaji yao kupitia mifumo ya ulemavu wa makuzi, huduma za afya, na elimu ya K-12. Familia zinaripoti kwamba zinapitia vikwazo vya rangi, vya kitamaduni, na vya lugha.**


## KIPAUMBELE CHA 2

Kusaidia kuhakikisha mashirika ya Usaidzi wa Awali wa Watoto Wachanga na Watoto Wadogo (ESIT) yanapata ufadhili wa Elimu Maalum kwa mwezi wa kwanza wa huduma zinazotolewa kwa familia.



Mashirika ya Usaidizi wa Awali yanapaswa kukamilisha hatua kadhaa kabla ya familia kuweza kuandikishwa na shirika kuweza kulipwa kwa fedha za Elimu Maalum. Watoa huduma wanafanya kazi ya kukusanya taarifa za familia, kufanya tathmini ya makuzi ya mtoto na ustahiki wake, kuandika ripoti, na kukutana na watoa huduma ya ulezi ili kuweka mipango ya huduma. Baada ya kazi yote hii, huduma huanza kwa watoto na familia, walakini mashiriki bado **hayawezi** kutumia fedha za Elimu Maalum kwa mwezi mmoja zaidi!

Mashirika ya Usaidizi wa Awali yanapaswa kukamilisha hatua kadhaa kabla ya familia kuweza kuandikishwa na shirika kuweza kulipwa kwa fedha za Elimu Maalum. Watoa huduma wanafanya kazi ya kukusanya taarifa za familia, kufanya tathmini ya makuzi ya mtoto na ustahiki wake, kuandika ripoti, na kukutana na watoa huduma ya ulezi ili kuweka mipango ya huduma.




Badiliko dogo la sheria hii linaweza kuongeza ufadhili kwa mashirika ya ESIT kwa kuyawezesha kutumia fedha za Elimu Maalum kwa mwezi wa kwanza wa huduma zinazotolewa kwa watoto wenye ustahiki. Bunge tu ndilo linaweza kufanya badiliko hili.

## KIPAUMBELE CHA 3

Kusaidia watu wenye I/DD kupata ajira na kudumu kazini, na kushirikishwa katika jumuiya zao, kwa kuongeza kiasi wanacholipwa watoa huduma za Ajira na Ujumuishaji katika Jumuiya.


Huduma za Ajira na Ujumuishaji katika Jumuiya zinawasaidia watu binafsi wenye I/DD kupata ajira na kudumu kazini na kuwa na ufikio na jumuiya yao. Watu wenye ajira pia wapo madhubuti kifedha, wanajitegemea zaidi, na wanachangia katika nguvukazi na uchumi, jambo linalomsaidia kila mtu. Watu wenye ajira na ufikio na jumuiya yao pia hunufaika kwa kupata marafiki wapya na kujifunza stadi mpya.

Watoa huduma za Ajira na Ujumuishaji katika Jumuiya wanaowasaidia watu kupata ajira na kudumu kazini katika jumuiya zao hawawezi kujaza nafasi zilizo wazi. Idara ya Huduma za Jamii na Afya (DSHS DDA) imeipa bunge upembuzi wa mwaka 2022 unaoelezea kiasi gani cha ufadhili ambacho watoa huduma wanakihitaji ili kujaza nafasi na kufidia gharama za huduma. Ikiwa bunge litatoa kiasi kilichopendekezwa kwenye upembuzi, basi 81% ya watoa huduma wa King County wanasema kwamba wanaweza kuhudumia kikamilifu washiriki wao wote wa sasa, na 86% wanasema wataweza kukubali washiriki wapya wanaotafuta ajira.


**Kila dola inayowekezwa katika usaidizi wa ajira ni sawa na faida ya senti 60 kwenye uchumi.**

**Kulingana na utafiti wa hivi karibuni wa watoa huduma, ikiwa idadi ingeongezwa hadi viwango pendelezwa, watoa huduma zaidi wangeweza kuhudumia kikamilifu washiriki wa sasa na kukubali washiriki wapya wanaotaka kuajiriwa.**

Kuhudumia kikamilifu washiriki wa sasa




Kukubali washiriki wapya wanaotaka kuajiriwa




Kulingana na utafiti wa hivi karibuni, 43% tu ya watoa huduma walisema kwamba kiwango cha sasa kinawawezesha kuhudumia washiriki kikamilifu.



## KIPAUMBELE CHA 4

Kusaidia kuhakikisha nyumba za gharama nafuu, na huduma ya usaidizi wa nyumba, zinapatikana kwa watu wenye I/DD.

Katika jimbo la Washington, takribani watu wazima 37,000 wenye ulemavu wa akili na makuzi (I/DD) wanakabiliwa na tatizo la makazi.

Watu wenye I/DD wanahitaji nyumba za gharama nafuu zenye huduma za usaidizi.

**Nyumba 37,000 za ziada zinahitajika kukidhi mahitaji haya ya nyumba**



**Nyumba 1,328 za HTF zimejengwa kwa ajili ya watu wenye IDD**

**Nyumba zilizopo kwa ajili ya watu wenye IDD zinakidhi 4% tu ya mahitaji yote.**
Makadirio ya uhitaji wa nyumba vs. nyumba maalum za IDD kutoka HTF, orodha ya jimbo lote.



**Mtu 1 kati ya 10 (11%) ambaye hana makazi katika jimbo la King County anaripotikiwa kuwa na IDD**

Mfuko wa Nyumba (HTF) ndiyo chanzo muhimu cha ufadhili wa miradi ya nyumba za gharama nafuu katika King County. Vyanzo vya kudumu vya ufadhili vinahitajika kwa HTF na chaguzi nyingine za nyumba mahalia na za Jimbo. Kwa kuunda vyanzo vya kudumu vya ufadhili na kuongeza fedha zaidi kwa HTF, Jimbo linaweza kuongeza nyumba zenye ufikio na gharama nafuu. Chaguzi za ufadhili mahalia wa nyumba pia zinahitajika. Hii inajumuisha matengenezo ya nyumba na fedha za utendaji kwa watoa huduma za nyumba wasio wa kutengeneza faida ili kuunga mkono umiliki wa muda mrefu.

Kwa suala la nyumba, ufikio ni jambo la msingi kwa watu wenye I/DD. Sehemu ya nyumba zinazofikika ni usaidizi unaotolewa na nguvukazi ya huduma za makazi katika jumuiya. Nguvukazi hii daima imekuwa ikifadhiliwa fedha zisizo toshelevu. Kulingana na Chama za Huduma za Makazi katika Jumuiya (CRSA), takribani 50% ya nguvukazi zenye uzoefu huacha kazi kila mwaka. Ongezeko la bei za watoa huduma litasaidia katika hili. Kufadhili wafanyakazi zaidi wa huduma za usaidizi wa nyumba katika DSHS DDA itasaidia kuboresha uratibu kati ya nyumba za makazi na huduma za usaidizi.

Jumuiya yetu inatuambia kwamba kutafuta nyumba ni jambo gumu. Jambo hili ni halisia hasa kwa familia za BIPOC ambazo lugha wanayozungumza nyumbani ni tofauti na Kiingereza.



**KIPAUMBELE CHA 5**

Kuajiri watoa huduma zaidi wa afya ya tabia na kuwapa mafunzo ya utaalamu wa kuhudumia kwa ufanisi zaidi watu wenye I/DD.


Watoa huduma wengi wa afya ya tabia hawana mafunzo na uzoefu maalum wa kuhudumia wenye I/DD na mahitaji ya afya ya tabia. Mafunzo maalum huwasaidia watoa huduma za afya ya tabia kugundua kwa usahihi na kusimamia dalili za watu hao, ambazo zinaweza kuwa tofauti kwa watu wenye I/DD. Mafunzo maalum yanaweza pia kufaa wakati wa matatizo ili kupunguza idadi ya watu wenye I/DD waliopelekwa vyumba vya dharura kwa ajili ya huduma za utengemano.



## SAUTI YA JUMUIYA

Wanajumuiya waliripoti katika kikao cha usikilizaji wa jumuiya kilichoandaliwa na King County kwamba huduma za afya ya tabia kwa watu wenye I/DD ni ngumu kupatikana na mara nyingi hazitolewi kwa watu wanaozungumza lugha yao na wanaoufahamu utamaduni wao.

Njia moja ya kuongeza idadi ya matabibu wa afya ya tabia wenye mafunzo maalum ni kufadhili malipo ya mikopo ya wanafunzi na programu za misamaha kwa wale wanaobobea katika I/DD. Njia nyingine ya kuongeza matabibu ni kuwapa mafunzo watoa huduma za sasa jinsi ya kutambua na kutibu watu wenye I/DD na mahitaji ya afya ya tabia.



**Takribani watu 2 katika kila watu 5 (37%) wenye ustahiki wa huduma za DDA katika Jimbo la Washington pia wana uhitaji wa matibabu ya afya ya tabia.**

Wanajumuiya waliripoti katika kikao cha usikilizaji wa jumuiya kilichoandaliwa na King County kwamba huduma za afya ya tabia kwa watu wenye I/DD ni ngumu kupatikana na mara nyingi hazitolewi kwa watu wanaozungumza lugha yao na wanaoufahamu utamaduni wao.